VERMONT
DEPARTMENT OF TAXES

# Muamana wa Kodi ya Jengo

Muamana wa Kodi ya Jengo wa Vermont huwasaidia wamiliki wengi wa nyumba wa Vermont kulipa kodi ya majengo. Unaweza kustahiki kupata muamana wa kodi ya majengo kwenye kodi yako ya majengo kama jengo lako linastahiki kuwa nyumba iliyozungukwa na shamba na unakidhi masharti ya kustahiki. Kiwango cha juu cha muamana ni $5,600 kwa ajili ya sehemu ya kodi ya majengo ya elimu ya Jimbo na $2,400 kwa sehemu ya kodi ya majengo ya manispaa.

## Kustahiki

Ili kuwasilisha muamana wa kodi ya majengo, lazima ukidhi masharti yafuatayo YOTE ya ustahiki:

- Majengo yako yamekidhi vigezo kuwa nyumba iliyozungukwa na shamba, na umewasilisha Tamko la Nyumba iliyozungukwa na shamba kwa ajili ya orodha kuu ya mwaka huu.
- Uliishi Vermont kwa mwaka mzima unaotozwa kodi.
- Hukudaiwa kama mtegemezi wa mlipakodi mwingine.
- Ulimiliki na kuishi katika majengo kama nyumba yako iliyozungukwa na shamba kuanzia tarehe 1 Aprili.
- Ukitimiza masharti haya, isipokuwa kama nyumba yako iliyozungukwa na shamba imepangishwa kwa mpangaji kuanzia tarehe 1 Aprili, bado unaweza kuidai kuwa nyumba iliyozungukwa na shamba ikiwa haijapangishwa kwa zaidi ya siku 182 katika mwaka unaodai.
- Unakidhi vigezo vya mapato ya kaya (tazama fomu ya ukomo wa mapato ya mwaka huu).

## Jinsi ya Kuwasilisha

Unapaswa kuwasilisha fomu mbili zifuatazo ili kutuma maombi ya muamana wa kodi ya majengo. Unaweza kuwasilisha madai yako kwa njia ya kielektroniki kwenye myVTax kama uwasilishaji wa pekee au unapowasilisha ritani yako ya Kodi ya Mapato ya Vermont.

- Fomu HS-122, Tamko la Nyumba Iliyozungukwa na Shamba na Madai ya Kodi ya Majengo
- Sehemu A: Tamko la Nyumba Iliyozungukwa na Shamba
- Sehemu B: Madai ya Muamana wa Kodi ya Majengo
- Jedwali HI-144, Mapato ya Kaya. Fahamu jinsi ya kubaini mapato ya kaya yako.

Mwaka wa Kodi: 2023 Mapato ya Juu Kabisa ya Kaya: $128,000

Mwaka wa Kodi: 2022 Mapato ya Juu Kabisa ya Kaya: $134,800

Mwaka wa Kodi: 2021 Mapato ya Juu Kabisa ya Kaya: $136,900

Mwaka wa Kodi: 2020 Mapato ya Juu Kabisa ya Kaya: $138,500

Mwaka wa Kodi: 2019 Mapato ya Juu Kabisa ya Kaya: $138,250

Mwaka wa Kodi: 2018 Mapato ya Juu Kabisa ya Kaya: $136,500

Mwaka wa Kodi: 2017 Mapato ya Juu Kabisa ya Kaya: $147,500

Mwaka wa Kodi: 2016 Mapato ya Juu Kabisa ya Kaya: $141,000

## Tarehe za Mwisho Kuwasilisha

Tarehe ya mwisho kuwasilisha Madai ya Muamana wa Kodi ya Majengo ni tarehe ileile ya kuwasilisha ritani yako ya kodi ya mapato ya Vermont na Tamko la Nyumba Iliyozungukwa na Shamba, ambayo kwa kawaida ni Aprili 15. Ukiwasilisha Tamko lako la Nyumba Iliyozungukwa na Shamba kabla ya tarehe ya mwisho iliyoongezwa ya Oktoba 15, bado unaweza kuwasilisha Madai ya Muamana wa Kodi ya Majengo hadi Machi 31 ya mwaka unaofuata. Hata hivyo, ada ya kushughulikia ya $150 itakatwa kutoka kwenye muamana wako wa kodi ya nyumba. Baada ya Oktoba 15, muamana wowote wa kodi ya majengo utatumwa moja kwa moja kwa mwenye nyumba na si kwenye mji.

## Kurekebisha Madai

Ukiwasilisha Madai ya Muamana wa Kodi ya Majengo pamoja na Tamko lako la Nyumba Iliyozungukwa na Shamba, unaruhusiwa kurekebisha au kubadilisha taarifa ifuatayo iliyotolewa kwenye fomu HS-122, Tamko la Nyumba Iliyozungukwa na Shamba na Madai ya Muamana wa Kodi ya Majengo na HI-144, Mapato ya Kaya, mradi tu Marekebisho yanafanywa ndani ya miaka mitatu ya tarehe ya mwisho ya kuwasilisha ya Aprili:

- mapato ya kaya,
- thamani ya eneo linaloizunguka nyumba,
- kodi ya elimu ya eneo linaloizunguka nyumba,
- kodi ya manispaa ya eneo linaloizunguka nyumba, na
- asilimia ya umiliki

Iwapo hutawasilisha ritani yako iliyorekebishwa kwa njia ya kielektroniki, unaweza kutumia Jedwali HI-144, Mapato ya Kaya, kwa mwaka husika ili kurekebisha mapato ya kaya. Ingiza mapato sahihi ya kaya na uweke alama IMEREKEBISHWA kwenye HI-144. Tuma HI-144 iliyorekebishwa bila kuchanganya na ritani nyingine yoyote inayowasilishwa katika Idara.

Tuma ritani yako kwa:

**Idara ya Kodi ya Vermont**

**P.O. Box 1645**

**Montpelier, VT 05601-1645**

## Fomu na Mwongozo wa Kodi

**Maelekezo ya myVTax**

- [Mwongozo wa myVTax wa Jinsi ya Kuwasilisha Tamko la Nyumbani Iliyozungukwa na Shamba au Madai ya Muamana wa Kodi ya Majengo (myVTax Guide How to File a Homestead Declaration or Property Tax Credit Claim)]

**Fomu na Maelekezo ya Kodi**

Tazama hapa chini kupata fomu, maelekezo na kikokotoo cha mikopo ya kodi ya majengo kilichotolewa na idara kwa urahisi wa walipa kodi na watayarishaji ili kukadiria kiasi cha Muamana wa Kodi ya Majengo ambacho mlipa kodi anaweza kupokea katika mwaka ujao wa kodi.

- Kijitabu cha Ritani ya Kodi ya Mapato ya Vermont: Kijitabu hiki kinajumuisha fomu na maelekezo ya: IN-111, IN-112, IN-113, IN-116, HS-122, RCC-146, HI-144 (Vermont Income Tax Return Booklet: This booklet includes forms and instructions for: IN-111, IN-112, IN-113, IN-116, HS-122, RCC-146, HI-144)
- HS-122, HI-144, Tamko la Nyumba Inayozungukwa na Shamba ya Vermont NA Madai ya Muamana wa Kodi ya Majengo (HS-122, HI-144, Vermont Homestead Declaration AND Property Tax Credit Claim) na Maelekezo (Instructions)
- HS-122, Kikokotoo cha Muamana ya Kodi ya Majengo (HS-122, Property Tax Credit Calculator)
- HS-122W, Tamko la Nyumba Iliyozungukwa na Shamba ya Vermont na/au Kutoa Muamana wa Kodi ya Majengo (HS-122W, Vermont Homestead Declaration and/or Property Tax Credit Withdrawal)

**Jarida na Mwongozo**

- Bili za Kodi na Usiri wa Taarifa za Marekebisho ya Kodi ya Majengo (Tax Bills and Confidentiality of Property Tax Adjustment Information)
- Muamana wa Kodi ya Majengo ya Vermont (The Vermont Property Tax Credit)
- Mfadhili wa Bili ya Majengo ya Vermont (Vermont Property Bill Backer)
- Jedwali la Vermont HI-144: Kubaini Mapato ya Kaya (Vermont Schedule HI-144: Determining Household Income)
- Taarifa ya Kodi ya Vermont kwa Wamiliki wa Nyumba Chini ya Mkataba wa Ruzuku ya Nyumba (Vermont Tax Information for Owners of Housing Subject to a Housing Subsidy Covenant)
- Kodi ya Wastaafu na Majengo: Unachopaswa Kujua (Veterans and Property Taxes: What You Should Know)

**Sheria, Kanuni na Taratibu**

- Kanuni ya § 1.5401(7) Nyuma Iliyozungukwa na Shamba (Regulation § 1.5401(7) Homestead)
- Kanuni ya § 1.5811(11)(A)(i), §1.5401(7), (14), §1.6066(c) Makazi (Regulation § 1.5811(11)(A)(i), §1.5401(7), (14), §1.6066(c) Domicile)
- Taarifa ya Kiufundi 20: Madai ya Marehemu (Technical Bulletin 20: Claims of Decedents)
- Taarifa ya Kiufundi ya 51: Marekebisho ya Jedwali la Mapato ya Jumla Yaliyorekebishwa HI-144 (Technical Bulletin 51: Adjustment to Modified Gross Income Schedule HI-144)
- *Taarifa ya Kifundi 56 (Inapitiwa): Kuripoti Mapato ya Biashara, Mapato ya K-1, Mapato ya Kodi na Mapato ya Mtaji kwenye Jedwali HI-144 Mapato ya Kaya (Technical Bulletin 56 (Under Review): Reporting Business Income, K-1 Income, Rental Income and Capital Gain on Schedule HI-144 Household Income)*